

**SHULE ZA ANESTAR**  
**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA- 2022**  
**KISWAHILI KIDATO CHA TATU**  
**KARATASI YA TATU (FASIHI)**  
**MUDA; SAA 2<sup>1/2</sup>**

**JINA.....DARASA.....NAMBARI.....**

**MAAGIZO: Jibu maswali yote katika karatasi hii**  
**SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI.**

1. a) Eleza umuhimu wa nyimbo katika usimulizi wa hadithi. (al.4)
- **KUburudisha hadhira**
  - **Huvuta hisia za hadhira**
  - **Huodoa ukinaifu**
  - **Husisitiza ujumbe katika hadithi**
  - **Huelimisha hadhira. (zozote 4 x 1 4)**
- b) i) Eleza maana ya misimu. (al.2)
- **Misimu ni misemo inayohusishwa na kundi ndogo la watu na huzuka katika kipindi cha wakati.**
- ii) Taja mifano yoyote miwili ya misimu. (al.2)
- **Beste – rafiki**
  - **Sare – kubebwa kwenye matatu bila kulipa**
  - **Ashuu – shilling kumi**
  - **Matatu/ Daladala – gari la uchukuzi wa umma**
  - **Boda – pikipiki/ baikeli inayobeba kwa malipo. (mwalimu ahakiki majibu ya mwanafunzi yoyote 2 x 1=2)**
- c) Taja sifa tatu za vitanza ndimi. (al.3)
- **Huwa kauli zinazokangabya kimatamshi**
  - **Huwa ni mchezo wa maneno**
  - **Huundwa kwa sauti zinazokaribiana kimatamshi**
  - **Hutumia maneni yenye maana zaidi ya majoa au zenye sauti sawa.**
- d) Taja sifa tatu za vitendawili. (al.3)
- **Lugha huwa ya kimafumbo**
  - **Hutumia lugha ya istiara**
  - **Huwa na mianzo maalumu**
  - **Aghalabu huegemea mazingira**
  - **Huwa fupi (3x1 =3)**
- e) Fafanua umuhimu wa vitendawili. (al.6)
- **Huburudisha hadhira**
  - **Huelimisha jamii**
  - **Hukuza ewezo wa kufikiri**
  - **Huhifadhi historia ya jamii**
  - **Hukuza ubunifu**
  - **Hutambulisha mazingira**
  - **Hukejeli tabia zisizokubalika. (6x1=6)**

**SEHEMU YA B: USHAIRI.**

*Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yote.*  
Akosaye shukurani, zako juhudi hajali,  
Hata nfanyie nini, haoni huyo hajali,  
Hata mpe milioni, matusi ndio stahili,  
Aona huna akili, ni yeye ndiye mshindi.

Patia kila la shani, bure unajisumbua,  
Takuona kama nyani, tena atakunyambua,  
Akuona punguani, chochote hutaambua,  
Usingoje shukurana, tenda wema wende zako.

Utafute kwa juhudi, bila kukata tama,  
Mpe apate faidi, wala asipate njaa,  
Hatachoka kukaidi, atakuletea balaa,  
Na mawazo yakujaa, maishayo hafikiri.

Mpe vyote vya haluwa, wenzako wamtamani,  
Hatakupa ya muruwa, juhudi haioni,  
Ataka kuzidishiwa, asubuhi na jioni,  
Ufanyacho hathamini, aongeze ya karaha.

Si ndugu wa si mwana, si rafiki si jirani,  
Shukrani kiwa hana, jua uko hatarini,  
Hadharani tatukana, aulize ndiwe nani,  
Ambe kama hajaona, kinyangarika kamawe.  
Hebu yeye msaili, amepata toa nini?  
Haweziye kukubali, kukupa hata thamani,  
Ni bure wake ukali, akutia mashakani,  
Yake wala hayaoni, mwovu hana shukurani.

Mfadhili watengaje, jana alikuopoa,  
Mwema wambwekeaje, mabaya wayachokoa,  
Mzazi wadharauje, mbali alishakutoa,  
Sasa jaribu kupoa, ujifunze shukurani.

### **Maswali**

1. Lipe shairi hili anwani mwafaka. (al.1)

**Mkosa shukurani hajali/ mkosa shukurani**

2. Hili ni shairi la aina gani? Thibitisha. (al. 4)

**Tarbia – lina mishororo minne kila ubeti**

**Mathawi – lia vipande viwili kila mshororo**

**Ukaraguni – vin avinambadirika ubeti hadi mwingine**

**Hutanja (1mk) Kuthibitisha(1mk) 1 x2 =2)**

3. Eleza dhamira ya mshairi katika shairi hili. (al. 2)

**Tujifunze kutoa shukurani kwa wenzetu waliotutenda mema ili tuimarisha uhusiano mzuri nao.**

4. Bainisha mifano mitatu ya uhuru wa mshairi katika shairi hili. (al.6)

- **Inkisari – takuona badala ya atakuona/ maishayo baa badala ya balaa**
- **Tabdila – haluwa badaa yah aula, Muruwa badala ya murua**
- **Kubananga/ kuboronga sarufi – zako juhudi hajali – hajali juhudi zako - bure unajisumbua – unajisumbua bure**
  - **Utohozi – milioni - million**

5. Andika ubeti wan ne kwa lugha nathari. (al. 4)

- Hata uki,pa vyovyote vitamu vinyowafanya wenzako waonee wivu hawezi kuonyesha wema wala kutambua juhundi zako. Yeye hutaka kupewa zaidi kila wakati. Kila unachokifanya hakithamini bali huongeza usumbufu.

6. Taja na utolee mfano tamathali zozote mbili za usemi katika shairi. (a1.4)

**Tabaine – si rafiki si jirani/ si ndugu si mwana**

**Tashbihi – takuona kama nyani**

**Msemo – Tenda wema nenda zako**

**Balagha – hebu yeye msaili amepata toa nini?**

7. Eleza maana ya neno hili kama lilivyotumika katika shairi hili. (a11)

Shani - ajabu

